

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO



MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA TANO

12 APRILI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA TANO– TAREHE 12 APRILI, 2022

I. DUA

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:


WAZIRI MKUU:


Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-


1. Toleo Na.05 la tarehe 04 Februari, 2022;
2. Toleo Na.06 la tarehe 11 Februari, 2022;
3. Toleo Na.07 la tarehe 18 Februari, 2022;
4. Toleo Na.08 la tarehe 25 Februari, 2022;
5. Toleo Na.09 la tarehe 04 Machi, 2022;
6. Toleo Na.10 la tarehe 11 Machi, 2022;
7. Toleo Na.11 la tarehe 18 Machi, 2022;
8. Toleo Na.12 la tarehe 25 Machi, 2022; na
9. Toleo Na.13 la tarehe 01 Aprili, 2022.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

- (a) Ripoti ya Mwaka ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 (*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Central Government for the Financial Year 2020/2021*);
- (b) Ripoti ya Mwaka ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 (*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Development Projects for the Financial Year 2020/2021*);
- (c) Ripoti ya Mwaka ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 (*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Public Authorities and Other Bodies for the Financial Year 2020/21*);
- (d) Ripoti ya Jumla ya Mwaka ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi kwa Kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi, 2022 (*The Annual Report of the Controller and Auditor General on the Performance Audit for the Period ending 31st March, 2022*);

- 
- (e) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Fedha na Usimamizi wa Mifuko na Programu za Serikali za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (*Performance Audit Report on Financing and Management of Government Funds and Programs*);
- (f) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo ya Ujenzi inayotekelezwa kwa Fedha za Mikopo (*Performance Audit Report on the Management of Construction Development Projects Financed Through Loans*);
- (g) Ripoti ya Ufuatiliaji wa tekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi zilizofanyika na kuwasilishwa Bungeni Mwezi Aprili, 2017 (*Follow – Up Report on the Implementation of the Controller and Auditor General’s Recommendations for the Performance Audit Reports issued and tabled before the Parliament in April, 2017*);
- (h) Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 (*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Local Government Authorities for the Financial Year 2020/2021*);

- 
- (i) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika ya Usimamizi na Uhifadhi wa Mifumo ya Ekolojia ya Ardhi Oevu (*Performance Audit Report on the Management of Conservation and Protection of Wetland Ecosystems in Tanzania*);
- (j) Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 (*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Information Systems for the Financial Year 2020/2021*);
- (k) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi na Utoaji wa Huduma za Miundombinu ya Mahabusu na Magereza (*Performance Audit Report on Administration and Provision of Remands and Prisons Infrastructure*);
- (l) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (*Performance Audit Report on the Allocation and Disbursement of Higher Education Students' Loans*);
- (m) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni (*Performance Audit Report on the Business Registration and Licensing*);

- 
- (n) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Utekelezaji wa Udhhibiti wa Shughuli za Vipimo (*Performance Audit Report on Implementation of Control Activities on Measurements*);
- (o) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mifumo ya Haki Jinai (*Performance Audit Report on the Criminal Justice System in Tanzania*);
- (p) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Ukarabati wa Barabara (*Performance Audit on the Management of Maintenance of Roads*);
- (q) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mapato katika Sekta ya Madini (*Performance Audit Report on the Management of Mechanisms for Revenue Collection in the Mining Sector*);
- (r) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Uendeshaji na Utangazaji wa Sekta ya Utalii Nchini (*Performance Audit Report on the Development and Promotion of Tourism Sector in Tanzania*);
na
- (s) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Makumbusho na Maeneo ya Urithi wa Utamaduni Nchini (*Performance Audit Report on the Management of National Museums and Cultural Heritage Sites in Tanzania*).

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

40. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Shule nyingine ya Msingi katika Kata ya Ng'ambo Tabora Mjini kwani Kata hiyo ni kubwa.

41. MHESHIMIWA OLIVER DANIEL SEMUGURUKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga njia mbili katika barabara ya Bandarini hadi Rwamishenyi na CRDB mpaka njia panda ya Kashai ili kuondoa msongamano.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

42. MHESHIMIWA OMAR ALI OMAR (WETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na uharibifu unaotokana na ukataji Mikoko na Uvunaji wa Matumbawe ili kuvinusuru visiwa visitoweke.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

43. MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunganisha mifumo ya Kitambulisho cha Mpiga Kura na Kitambulisho cha Taifa ili kuepusha usumbufu.

44. MHESHIMIWA HAJI AMOUR HAJI (PANGAWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itakarabati mtambo wa kielektroniki ulioharibika na kusababisha mrundikano wa hati za ukaazi Zanzibar.

WIZARA YA KILIMO:

45. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-


Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti kuongezeka kwa bei ya mbolea nchini hasa Mkoani Ruvuma.

WIZARA YA AFYA:

46. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa kuna vyumba maalum kwa ajili ya kujifungulia Wanawake wenye ulemavu.



WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

47. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa uwanja wa Ndege wa Sumbawanga Mjini.

WIZARA YA MAJI:

**48. MHESHIMIWA ALEXANDER PASTORY MNYETI
(MISUNGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji katika Mji wa Misasi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
12 APRILI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**